


EPISCOPAL CHURCH of the  
**HEAVENLY REST**

God's Love. For All.

---

Jumapili ya tisa baada ya Pentekoste  
Ibada kwa Kiswahili  
Jumapili, Agosti 7, 2022  
1:00 alasiri



Ninth Sunday after Pentecost  
Worship in Swahili  
Sunday, August 7th, 2022  
1:00 in the afternoon

## AGANO LA KALE

Isaya 1:1, 10-20

Haya ni maono ya Isaya, mwana wa Amози, aliyoyaona katika habari za Yuda na Yerusalemu, siku za Uzia na Yothamu na Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda. Lisikieni neno la Bwana, enyi waamuzi wa Sodoma; tegeni masikio msikie sheria ya Mungu wetu, enyi watu wa Gomora. Huu wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani? Asema Bwana. Nimejaa mafuta ya kafara za kondoo waume, na mafuta ya wanyama walionona; nami siifurahii damu ya ng'ombe wala ya wana-kondoo wala ya mbuzi waume. Mjapo ili kuonekana mbele zangu, ni nani aliyetaka neno hili mikononi mwenu, kuzikanyaga nyua zangu? Msilete tena matoleo ya ubatili; uvumba ni chukizo kwangu; mwezi mpya na sabato, kuita makutano; siyawezi maovu hayo na makutano ya ibada. Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa, nafsi yangu yazichukia; mambo hayo yanilemea; nimechoka kuyachukua. Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho yangu nisiwaone; naam, mwombapo maombi mengi, sitasikia; mikono yenu imejaa damu. Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane. Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi; bali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga; maana kinywa cha Bwana kimenena haya.

Hilo ndilo Neno la Bwana.

**Asante kwa Bwana.**

## AGANO JIPYA

Waebrania II:1-3, 8-16

Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa. Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri. Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu. Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba; alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu. Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika. Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakazona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi. Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe. Na kama wangaliikumbuka nchi ile waliyotoka, wangalipata nafasi ya kurejea. Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji.

Hilo ndilo Neno la Bwana.

**Asante kwa Bwana.**

## HABARI NJEMA

Luka 12:32-40

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa Yohana.

**Utukufu uwe nawe, Ee Bwana wetu.**

Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na mioyo yenu. Viuno vyenu na viwe vimefungwa, na taa zenu ziwe zinawaka; nanyi iweni kama watu wanaomngojea bwana wao, atakaporudi kutoka arusini, ili atakapokuja na kubisha, wamfungulie mara. Heri watumwa wale, ambao bwana wao ajapo atawakuta wanakesha. Amin, nawaambieni, atajifunga na kuwakaribisha chakulani, atakuja na kuwahudumia. Na akija zamu ya pili, au akija zamu ya tatu, na kuwakuta hivi, heri watumwa hao. Lakini fahamuni neno hili, Kwamba mwenye nyumba angalijua saa atakayokuja mwivi, angalikesha, wala asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. Nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa saa msiyodhani ndipo ajapo Mwana wa Adamu.

Hii ndiyo Habari Njema ya Kristo.

**Tunakusifu sana, Ee Kristo, Kwa Habari Njema takaifu.**

## FIRST READING

Isaiah 1:1, 10-20

The vision of Isaiah son of Amoz, which he saw concerning Judah and Jerusalem in the days of Uzziah, Jotham, Ahaz, and Hezekiah, kings of Judah. Hear the word of the Lord, you rulers of Sodom! Listen to the teaching of our God, you people of Gomorrah! What to me is the multitude of your sacrifices? says the Lord; I have had enough of burnt offerings of rams and the fat of fed beasts; I do not delight in the blood of bulls, or of lambs, or of goats. When you come to appear before me, who asked this from your hand? Trample my courts no more; bringing offerings is futile; incense is an abomination to me. New moon and sabbath and calling of convocation-- I cannot endure solemn assemblies with iniquity. Your new moons and your appointed festivals my soul hates; they have become a burden to me, I am weary of bearing them. When you stretch out your hands, I will hide my eyes from you; even though you make many prayers, I will not listen; your hands are full of blood. Wash yourselves; make yourselves clean; remove the evil of your doings from before my eyes; cease to do evil, learn to do good; seek justice, rescue the oppressed, defend the orphan, plead for the widow. Come now, let us argue it out, says the Lord: though your sins are like scarlet, they shall be like snow; though they are red like crimson, they shall become like wool. If you are willing and obedient, you shall eat the good of the land; but if you refuse and rebel, you shall be devoured by the sword; for the mouth of the Lord has spoken.

The Word of the Lord

**Thanks be to God.**

## SECOND READING

Hebrews 11:1-3, 8-16

Now faith is the assurance of things hoped for, the conviction of things not seen. Indeed, by faith our ancestors received approval. By faith we understand that the worlds were prepared by the word of God, so that what is seen was made from things that are not visible. By faith Abraham obeyed when he was called to set out for a place that he was to receive as an inheritance; and he set out, not knowing where he was going. By faith he stayed for a time in the land he had been promised, as in a foreign land, living in tents, as did Isaac and Jacob, who were heirs with him of the same promise. For he looked forward to the city that has foundations, whose architect and builder is God. By faith he received power of procreation, even though he was too old-- and Sarah herself was barren-- because he considered him faithful who had promised. Therefore from one person, and this one as good as dead, descendants were born, "as many as the stars of heaven and as the innumerable grains of sand by the seashore." All of these died in faith without having received the promises, but from a distance they saw and greeted them. They confessed that they were strangers and foreigners on the earth, for people who speak in this way make it clear that they are seeking a homeland. If they had been thinking of the land that they had left behind, they would have had opportunity to return. But as it is, they desire a better country, that is, a heavenly one. Therefore God is not ashamed to be called their God; indeed, he has prepared a city for them.

The Word of the Lord

**Thanks be to God.**

## THE GOSPEL

Luke 12:32-40

The Holy Gospel of our Lord Jesus Christ according to Luke.

**Glory to you, Lord Christ.**

Jesus said to his disciples, "Do not be afraid, little flock, for it is your Father's good pleasure to give you the kingdom. Sell your possessions, and give alms. Make purses for yourselves that do not wear out, an unfailing treasure in heaven, where no thief comes near and no moth destroys. For where your treasure is, there your heart will be also. "Be dressed for action and have your lamps lit; be like those who are waiting for their master to return from the wedding banquet, so that they may open the door for him as soon as he comes and knocks. Blessed are those slaves whom the master finds alert when he comes; truly I tell you, he will fasten his belt and have them sit down to eat, and he will come and serve them. If he comes during the middle of the night, or near dawn, and finds them so, blessed are those slaves. "But know this: if the owner of the house had known at what hour the thief was coming, he would not have let his house be broken into. You also must be ready, for the Son of Man is coming at an unexpected hour."

The Gospel of the Lord.

**Praise to you, Lord Christ.**



---

602 Meander Street Phone: (325) 677-2091  
Abilene, Texas 79602 Email: [info@heavenlyrestabilene.org](mailto:info@heavenlyrestabilene.org)  
Website: [heavenlyrestabilene.org](http://heavenlyrestabilene.org) Social media: [@heavenlyrestabilene](https://www.facebook.com/heavenlyrestabilene)

#### CLERGY AND STAFF

The Reverend David F. Romanik, <i>Rector</i>	Blaine Beyer, <i>Director of Communications</i>
The Reverend Corrie Cabes, <i>Assistant Rector</i>	Steve Gibbs, <i>Parish Coordinator</i>
The Reverend Amanda Watson, <i>Assisting Priest</i>	LeighAnna Morris, <i>Parish Accountant</i>
The Reverend Dr. Doug Thomas, <i>Priest in Residence</i>	Nolan Kelley, <i>Verger</i>
The Reverend Karen Boyd, <i>Deacon</i>	Sharon Kelley, <i>Hospitality and Kitchen Coordinator</i>
The Reverend Dr. Russell Dickerson, <i>Deacon</i>	Robert Becerra, <i>Sexton</i>
Bikole Mulanda, <i>Swahili Minister</i>	Adrian Smith, <i>Assistant Sexton</i>
Jesse Ratcliffe, <i>Organist and Director of Music</i>	Dorothy Guerra, <i>Housekeeper</i>
Shelly Reed, <i>Children's Music Assistant</i>	Anne Jones, <i>Nursery Manager</i>
Carol Ann Weston, <i>Director of Family Ministries</i>	

#### VESTRY AND APPOINTED OFFICERS

Judy Godfrey, *Senior Warden*; Rick Willis, *Junior Warden*; Debbie Sherman, *Secretary*; Connie Collier, Sarah Ferguson, Lori Houghtalen, Annabel House, Harry Hurt, Mike Langford, Robert Peterson, Darryl Tippens, John Walton, Steve Suttle, *Chancellor*; and Sam Cutbirth, *Treasurer*

---